

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
31 Oktoba 2009**

Waliohudhuria

Solomon Mihoyo
Filbert Mbecha
Dominata Rwechungura
George Kabogo
Selion Elieskia
Shamte J Kisoma
Sosthenes C Amlima
Elaine Baker-Guni
Beda John Mkusu
Abdul H Mwaibambe
Juma Ali Salehe Jongo
Abdala Ally Majaliwa
Mohammed Samwely
Edgar R Paulo
Paulo Atibu Hatibu
Othmani Mussa Kitemo
Hamza Mohamed
Hamadi Hatibu Bwaja

Msafara

Msafara ulianda vizuri. Tulipata taarifa kwamba siku hiyo ilikuwa siku ya kampeni ya mabadaliko ya tabia ya nchi ya www.350.org basi tuliunganisha msafara na kampeni hiyo. Mgeni Rasmi Waziri wa Nchi kwenye ofisi ya makamu rais alikuwepo na wageni kutoka TANROADS, traffic police na Diwani Lupilya walishiriki kwa kuendesha baisikeli kwenye msafara. Watu wa East Africa TV walikuwepo. Dominata alileta gazeti ya Sunday News (tulikuwepo kurasa la kwanza) na gazeti la Nipashe (picha ilikuwepo). Msafara wa Rais ulitupita na Rais alituona. Elaine alitumia picha kwa 350.org na waliweka makala kuhusu msafara wetu kwenye website yao.

Tuliamua kuandika barua za kushukuru kwa British High Commission, Kampuni ya Guta, Waziri wa Nchi ofisi ya makamu rais, TANROADS, Traffic Police na Diwani Lupilya.

Bwana Mengi alijibu barua kusema hataweza kuhudhuria.

Filbert atatengeneza repoti ya kifedha ya msafara.

Ride Planet Earth

Tulikubali kufanya msafara ndogo siku ya Ride Planet Earth tarehe 6 mwezi wa 12.

UNDP

Edgar alimpa Elaine namba ya ndugu yake ofisi ya UNDP na Elaine aliongea naye na tutakutana naye jumatano.

Tunaweza kuomba hela ya:

- msafara wa tarehe 8 mwezi wa 12
- kuendelea na mradi wa Wamba
- kongamano
- mafunzo ya kompyuta
- mafunzo mengine
- kodi ya ofisi
- ada ya website
- camera
- meza, hema na vifaa vya ofisi
- projector
- msaada wa kuanzisha UWABATAN

Foundation Civil Society

Elaine atawatumie email kuomba mkutano nao.

Laptop

Natalie, rafiki wa Elaine, alitupa laptop yenye keyboard mbovu. Elaine atajaribu kurekebisha ili tutumie ofisini.

Website

Elaine aliweka taarifa kwenye website kuhusu msafara, Mbeya, UWABATAN na semina ya waalimu wa udereva.

Mradi wa Wamba - Wiki ya Usalama Barabarani – Mbeya

Dominata na Sosthenes walimaliza repoti na Dominata alisoma. Elaine atachapa.

Tanga

Tunasubiri Hussein Hamza asahihishe dondoo.

Idrisa wa Tanga alisema wanaendelea vizuri kusanya documents na barua.

Amend na siku ya kuwakumbuka wahanga wa ajali za barabarani

Mejah na Dominata wanaendelea kushirikiana na Amend. Watahudhuria mkutano mwingine jumatatu.

Fasta Cycle Messenger Cooperative

Elaine alisahihisha masharti. Filbert na Hamadi watayapeleka ofisi ya Bwana Bukuku ili apitie kuona kama kuna matatizo.

Uchaguzi wa 2010

Elaine atatararisha barua kwenda vyombo vya habari.

Mkutano wa Barabara Arusha

Elaine aliwakumbusha lakini hatujapata jibu. Bwana Haule alisema tunaweza kutumia tena fomu kutoka ofisi yake. Elaine atapata taarifa ofisi yake iko wapi.

Mikutano na Meya na Waziri

Elaine atatoa tena barua ili tufuatalie.

Climate Change Forum

UWABA tumealikwa kujiunga na Climate Change Forum na wawakilishi wawili kuhudhuria mkutano tarehe 11 mwezi wa 11. Elaine na Mejah watahudhuria.

Tunamsubiri Mejah

Re-cycle

Wimbo

Kadi ya benki

Filbert atakuja na dondoo za uchaguzi wa kamati zimezosainiwa ili wengine wasaini.

Hela na guta

Wote tumempa risiti Filbert lakini Mejah bado. Filbert alitumia Tsh 36,000 kwa ajili ya chakula cha wanachama baada ya msafara.

Tsh 200,000 imebaki kwenye badjeti ya maji – Edgar atarudisha wiki ijayo. Pia Tsh 100,000 imebaki kwenye badjeti ya baisikeli – Filbert anayo. Tsh 5,000 ilibaki kwenye badjeti ya photocopy (Elaine).

Dereva wa guta (Ramadhani) alilipa Tsh 14,000 sasa anadaiwa Tsh 13,000.

Mejah anadai Tsh 13,000.

Filbert alimpa Dominata Tsh 1,000 ya kununua gazeti na Paulo Tsh 8,000 ya ulinzi. Hela zingine za ulinzi Elaine alichangia kutoka hela zake binafsi.

Tulimaliza posho ya Juma ya mwezi wa kumi Tsh 10,000.

Elaine alirudishiwa Tsh 160,250 (Tsh 165,250 minus Tsh 5,000 ya badjeti ya photocopy). Sasa hadai wala hadaiwi.

Hussein Hamza anadaiwa Tsh 10,000.

Idrisa hajarudisha hela za Morogoro bado (Tsh 40,000).

Filbert sasa ana Tsh 35,000 ya hela ya msafara na Tsh 14,500 ya hela ya kawaida ya UWABA.